



Darasa la

1

Kitabu cha hadithi 4

Kiswahili

- ★ **Kwa nini Mzee Kobe ana magamba**
- ★ **Jitu la mtoni**



Tusome Early Literacy Programme

Kwa nini Mzee Kobe ana magamba


Mwandishi: **Silas Emolem**

Mchoraji: **Simon Ndonge**

Hapo zamani za kale, palikuwa na mnyama aliyeitwa Mzee Kobe.

Mzee Kobe alikuwa rafiki wa ndege wawili.





Marafiki hawa walitembea pamoja.

Walienda katika sherehe pamoja.

Siku moja ndege walimualika Mzee Kobe kwenye harusi.

Mzee Kobe alifurahi sana.

Siku ya harusi marafiki hao walijipamba sana.

Kobe hakuweza kupaa angani.

Ndege walimwambia Mzee Kobe kuwa wangembeba.

Ndege walichukua kipande cha mti na kukishika kwa midomo yao.

Mzee Kobe akakikalia kipande hicho cha mti.



Wakiwa angani kipande cha mti
kilivunjika.

Mzee Kobe alianguka juu ya mawe.

Mgongo wake ukapasukapasuka
sana.

Mgongo wake ulipoona, ukawa
na magamba.





Tangu siku hiyo Kobe akawa na magamba kwenye mgongo wake.

Maswali

1. Ndege walimualika Mzee Kobe wapi?
2. Ndege walitumia nini kumbeba Mzee Kobe?
3. Mzee Kobe alianguka wapi?

Jitu la Mtoni

Mwandishi: **Nashera Ara Kodawa**

Mchoraji: **Simon Ndonye**

Katika kijiji cha Ngomongo, paliishi wasichana wawili.

Wasichana hao waliitwa Hana na Amina.

Wawili hao walipenda sana kuogelea.





Siku moja Hana na Amina walienda kuogelea mtoni.

Amina aliokota kichupa kidogo mle majini.

Hana akamwambia Amina,
“Tukifungue tuone kuna nini ndani.”



Mara tu walipokifungua, kilitoa
moshi mweupe.

Ndani ya ule moshi kulikuwa na
jitu.

Amina na Hana waliogopa sana
wasijue la kufanya.

Kile kichupa kikaanza kutoa moshi tena.

Ndani ya ule moshi kulikuwa na msichana mrembo.

Amina na Hana wakamlilia awasaidie.



Yule msichana mrembo aliligeukia jitu.

Macho yao yalipolingana, lile jitu likageuka tena kuwa moshi likatoweka.

Tangu siku hiyo, Amina na Hana wakajifunza kuwa si vyema kuokota vitu ovyo.



Maswali

1. Amina na Hana waliishi wapi?
2. Nini kilitoka kwenye kichupa?
3. Ni nani aliyewasaidia Amina na Hana?

Darasa la 1

Kitabu cha hadithi 4

★ Kwa nini Mzee Kobe ana magamba

★ Jitu la mtoni

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

Hadithi katika msururu huu ni:

- Darasa la 1:**
- ▶ Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
 - ▶ Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
 - ▶ Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
 - ▶ Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

- Darasa la 2:**
- ▶ Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpandaye
 - ▶ Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
 - ▶ Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
 - ▶ Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
 - ▶ Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.